



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



TANGAZO KWA UMMA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoungwa kwa **Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339**. Bodi pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kutoa leseni ya Uendeshaji wa Ghala.

Bodi inapenda kuutaarifu Kampuni zenye nia ya kuendesha ghala **kwa msimu wa mwaka 2026/2027 wa mauzo ya zao la Karanga** kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwasilisha dhamira zao. Barua ya dhamira iambatane na nyaraka zifuatazo;

- i. Cheti cha usajili wa kampuni;
- ii. Hati ya uwanzishwaji wa kampuni (MEMARTS);
- iii. TIN na Leseni ya biashara;
- iv. Taarifa ya Mwaka ya Kampuni (Annual return)

Aidha Mleta dhamira atatakiwa kuainisha mkoa na wilaya anaotarajia kufanya kazi.

- v. Kithibitisho cha malipo ya ada ya usaili

Wakurugenzi wa kampuni zenye nia ya kuendesha ghala kwa zao la karanga watafanyiwa usaili tarehe **25 Mei 2026** kulingana na ratiba itakayotolewa kabla ya tarehe usaili. Usaili huo unatarajiwa kufanyika Mkoani Dodoma katika ofisi za bodi ya usimamizi wa stakabadhi za ghala, Kama kutakuwa na mabadiliko ya ukumbi tutawajulisha kwa taarifa rasmi.

Baada ya usaili kukamilika na matokeo kutangazwa, Kampuni zitakazokuwa zimefaulu ndizo zitakazoruhusiwa kuendelea na mchakato wa maombi ya leseni kwa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa hususani **kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339**.

Kwa kampuni zenye nia na vigezo husika, zinatakiwa kuwasilisha dhamira zao kupitia barua pepe **info@wrrb.go.tz** au Ofisi za Bodi zilizoko **Ghorofa ya 1, Kiwanja Na. 23 Kitalu Na. 3 Barabara ya Tembo, Mtaa wa Nyerere – Majengo, Dodoma**. Barua zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala. **Mwisho wa kuwasilisha dhamira ni tarehe 22 Mei 2026 saa 10:00 jioni.**

Kwa maelezo zaidi tafadhari wasiliana na **Bw. Emmanuel Mlenge** kwa simu namba **0683177007** au barua pepe **emmanuel.mlenge@wrrb.go.tz**

NB: *Kampuni ambayo haitawasilisha dhamira yake ndani ya muda uliopangwa haitaruhusiwa kushiriki kwenye usaili na itakosa sifa ya kuendesha Ghala la zao la karanga kwa msimu wa mwaka 2026/2027.*

Imetolewa na;
MKURUGENZI MTENDAJI
14 Mei 2026

